PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT

TANGAZO KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU NANE NANE 2019. .

Kuhusu Taasisi ya PASS-Tust.

Taasisi ya Private Agricultural Sector Support (PASS-Trust) ilianzishwa mwaka 2000 chini ya Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo, kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha na kibiashara kwa wajasiriamali wa bidhaa na huduma katika sekta ya kilimo nchini Tanzania.

Taasisi hii imefanya kazi kama mradi mpaka kufikia mwaka 2007 ambapo ilisajiliwa kama mfuko wa udhamini ikiwa na malengo yale yale.

Hivi sasa PASS inafanya kazi kama taasisi ikiwa kama kiungo kati ya sekta ya kilimo na sekta ya fedha. Lengo letu kuu ni kuwezesha upatikanaji wa huduma za maendeleo za kifedha na kibiashara kwa wajasiriamali wa biashara za kilimo katika mnyororo mzima wa biashara za kilimo.

Walengwa wa PASS:

Watu wanaohudumiwa na PASS ni pamoja na wajasiriamali binafsi wa biashara za kilimo, vyama / makundi ya wakulima wadogo wadogo na makampuni yanayojihusisha na sekta ya kilimo. Pamoja na mambo mengine, PASS inawasaidia wateja wake katika kuandaa mpango bora wa uwekezajiambao uwapatia faida kubwa na kuwezesha upatikanaji wa huduma za fedha kwa ajili ya kuifadhili miradi hiyo kupitia udhamini wa mikopo kwa kushirikiana na benki za kibiashara.

Hadi leo, PASS inafanya kazi na benki 16 zikiwemo. CRDB, NMB, TIB, BOA, ABC, AKIBA Commercial Bank, Amana bank, TADB, NBC, TPB, AZANIA bank LTD, Vision fund Microfinance Bank LTD, ACCESS Bank, Equity bank and Mkombozi Commercial Bank.

PASS inaendelea na mchakato wa kusaini makubaliano na mabenki zaidi ya biashara, pamoja na kusaidia upatikanaji wa mikopo (kutafuta fedha) kwa jamii pamoja na taasisi za fedha za vijijini.

Mafanikio Yetu:

Kwa namna tunavyofanya kazi katika kuunga mkono maeneo muhimu ya vipaumbele vya serikali hususan katika kutengeneza ajira na uwekezaji nchini, napenda kusema kuwa PASS inaendelea kuwa shirika la mfano ambalo kwa dhati kabisa limewawezesha wakulima wadogo wadogo kupata huduma za kifedha.

Jumla ya wajasiriamali wa kilimo 929,172 wamefaidika na mikopo iliyodhaminiwa na PASS inayofikia Shilingi bilioni 712 kati ya mwaka 2000 na 2018.

Wanufaika hawa wanatoka sekta mbali mbali, ambazo zinajumuisha mifugo, uzalishaji wa mazao, usindikaji, biashara ya mazao, vifaa vya kilimo, misaada ya miundombinu ya umwagiliaji, usafirishaji wa bidhaa za kilimo, ufugaji wa nyuki, ufugaji wa samaki pamoja na biashara ya pembejeo.

Katika mwaka wa 2018 pekee, PASS ilinufaisha jumla ya biashara 196,873 zinazojihusisha na mazao na huduma kwenye kilimo kupitia udhamini wa mikopo na huduma za maendeleo ya biashara katika mikoa 26 kote nchini. Mikopo hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha na kupanua wigo wa biashara za mazao na huduma katika kilimo nchini.

Katika mwaka huo huo, PASS ilidhamini mipango ya biashara 15,564 yenye thamani ya Shilingi bilioni 191 ambayo iliwasilishwa kwenye mabenki mbalimbali tunayoshirikiana nayo kwa ajili ya kuipatia fedha.

Katika kuwanufaisha vijana wa humu nchini, PASS kupitia kituo chake cha AgribusinessInnovation Centre (AIC) ambacho ndicho kituo chetu cha ubunifu, tunashirikiana na chuo kikuu cha Sokoine mkoani Morogoro na vile vile Tanzania Livestock Research Institute (TALIRI) katika kutoa mafunzo ya kibiashara kwa vijana.

Katika kuwawezesha vijana kubadili mitazamo na kilimo kwa vijana. Vijana wamewekwa katika mazingira maalumu wakijifunza masuala ya biashara katika kilimo cha mboga mboga (nyanya ndani ya kitaru nyumba) pamoja na mifugo, shabaha kuu ikiwa ni unenepeshaji wa mbuzi.

Mwezi ujao wa Septemba, takriban vijana 20 watafuzu kutoka kituo cha Morogoro ambako wamekuwa wakipata mwongozo wa kilimobiashara. Hali kadhalika, PASS - AIC iko katika harakati za kuingiza kundi la awamu ya pili, linalotarajiwa kuanza mwezi Octoba 2019 ambapo jumla ya vijana 70 wanategemewa kujiunga.

Huko Kongwa, programu ya unenepeshaji wa mbuzi inaendelea ambapo vijana wanapokea mwongozo kuhusu jinsi ya kuneepesha mbuzi kwa ajili ya mauzo.

PASS itaendelea kushirikiana na wadau mbali mbali ambao wametuwezesha kutimiza malengo yetu. Kwa kipekee tunatambua juhudi za wadau wetu World Food Program (WFP) kupitia kwa Farm to Market Alliance (FtMA) na Agricultural Markets Development Trust (AMDT) ambao wamefanya kazi ya kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wakulima wadogo wadogo katika kanda ya kusini. Vile vile shirika

la LIC na International Trade Centre kwa kutoa mafunzo kwa wafanyikazi katika kilimo biashara. Zaidi ya walengwa 7000 wamenufaika kutokana na mafundisho haya.

Aidha, PASS , mwishoni mwa mwezi Julai imetia saini mkataba kati yake na benki ya maendeleo ya Africa (AFDB), ambao utapelekea takriban wakulima 80,000 kuwezeshwa kujikinga kutokana na majanga ya asili na ambayo hayana kinga ya bima.

Aidha, PASS itaendelea kushirikiana na taasisi za kifedha katika kuhakikisha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima kwa ajili kuedeleza kilimo biashara.

Hitimisho:

Napenda kuwashukuru washirika wetu, benki washirika kwa kuwa na uelewa zaidi katika kusaidia uwekezaji kwenye kilimo kupitia huduma za kifedha. Lengo letu sasa ni kupanua huduma zetu ili watu wengi zaidi waweze kufaidika na huduma zetu.

2019 ni mwaka wa pili wa mpango mkakati wetu wa miaka mitano (2018-2022). Tumelenga kutengeneza ajira 700,000 kwa ujumla kwa njia ya moja kwa moja au kuptitia njia zingine katika sekta ya kilimo tukiwa na lengo la kuzinufaisha walau familia 235,253 kupitia udhamini wa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 210.6.

Asanteni sana

Nicomed Bohay

Mkurugenzi Mtendaji wa PASS